



THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

KISWAHILI SEHEMU (A)

Monitoring Learner Achievement at Primary School Level in Kenya

Gredi ya 4

NAKALA YA MWANAFUNZI



GLOBAL
PARTNERSHIP
for EDUCATION



REPUBLIC OF KENYA
MINISTRY OF EDUCATION



THE WORLD BANK
IBRD • IDA | WORLD BANK GROUP

Karatasi hii ina sehemu moja tu

Kusoma kwa Sauti

Mwalimu amwambie mwanafunzi aome kifungu kifuatacho kwa sauti.

Bwana na Bibi Mambo wana watoto wawili ambao ni Raha na Mwema. Wote hudumisha usafi. Wanatambua kuwa usafi ni muhimu katika maisha ya binadamu. “Usafi husaidia kuzuia magonjwa. Kila mtu lazima aoge, apige mswaki na kuvaa nguo safi kila siku,” Bwana Mambo huwakumbusha watu wa familia yake.

Wanashirikiana kufanya usafi wa mazingira yao. Wao hufyeka nyasi, hufagia, hupiga deki na hata kuosha na kupanga vyombo. Raha na Mwema hufagia chumba cha kuku kila siku. Nao Bwana na Bibi Mambo hufagia zizi la ng’ombe. Wakati mwingine Raha na Mwema huosha na kupanga vyombo kwa zamu. Bwana Mambo hukata nyasi zinapokua. Naye Bibi Mambo hupiga deki nyumba yao baada ya siku mbili.

“Hakikisheni kila mahali ni safi”, Bibi Mambo huwaambia Raha na Mwema kila wakati.